



Parenting Payment

Parenting Payment ni msaada wa kipato kwa wazazi au walezi ili kusaidia na gharama ya kulea watoto.

Parenting Payment ni malipo tofauti na Family Tax Benefit na Parental Leave Pay. Pia kuna malipo mengine kwa familia ambayo huenda unaweza kupata.

Ustahili kwa Parenting Payment

Parenting Payment inalipwa kwa mlezi mkuu wa mtoto.

Mzazi au mlezi mmoja pekee anaweza kupata malipo.

Unaweza kupata Parenting Payment kama mzazi, babu au bibi, au mlezi, ikiwa yoyote ya masharti haya yanatumika:

- wewe ni mseja (bila mwenzi) na unamtunza angalau mtoto mmoja mwenye umri chini ya miaka 14.
- una mwenzi na unamtunza angalau mtoto mmoja mwenye umri chini ya miaka 6.

Ili kupata malipo haya, utahitaji pia kukidhi sheria hizi:

- mapato na mali yako pamoja na ya mwenzi wako (kama unaye mmoja) ni chini ya kiasi fulani
- unakidhi mahitaji ya makazi
- unakidhi mahitaji ya wajibu wa pande zote ikiwa inahitajika.

Viwango vya malipo kwa Parenting Payment

Kiasi cha Parenting Payment unachopata kinategemea hali yako ya familia. Viwango hivyo vinasasishwa kwa tarehe 20 Machi na 20 Septemba kila mwaka. Ili kupata viwango vya hivi karibuni nenda kwa servicesaustralia.gov.au/parentingpayment

Vipimo vya mapato na vya mali kwa Parenting Payment

Kiasi cha Parenting Payment unachopata kinategemea mapato na mali yako pamoja na ya mwenzi wako (ikiwa unaye mmoja).

Mali ni mali au milki yoyote unayomiliki ama kwa sehemu au kamili. Inajumuisha mali uliyo nayo, nje ya Australia na pesa na madeni unayodaiwa. Vipimo vya mapato na vya mali vinasasishwa kwa tarehe 20 Machi, 1 Julai na 20 Septemba kila mwaka.

Ili kupata viwango vya hivi karibuni nenda kwa servicesaustralia.gov.au/parentingpayment

Jinsi ya kudai

Huwezi kuwasilisha madai kwa Parenting Payment kabla ya mtoto amezaliwa. Kwa kawaida tunatathmini Parenting Payment yako kuanzia tarehe unapowasilisha madai yako na hati zako.

Tunaweza kuhesabu malipo yako kuanzia tarehe ya nyuma ikiwa unawasilisha dai yako na hati zako ndani ya ama wiki 4 za:

- kuzaliwa kwa mtoto wako
- tarehe ambayo mtoto alikuja kwako kutunzwa.

Unaweza kuomba kwa malipo haya mtandaoni. Ili kupata maelezo nenda kwa servicesaustralia.gov.au/parentingpayment

Kwa habari zaidi

- nenda kwa servicesaustralia.gov.au/parentingpayment ili kupata maelezo zaidi katika Kiingereza
- nenda kwa servicesaustralia.gov.au/ftb ili kupata habari zaidi kuhusu Family Tax Benefit katika Kiingereza na lugha nyingine
- nenda kwa servicesaustralia.gov.au/yourlanguage unapoweza kusoma, kusikiliza au kutazama video yenye habari katika lugha yako
- piga simu kwa **131 202** kuongea nasi katika lugha yako kuhusu malipo na huduma ya Centrelink
- piga simu kwa **132 011** kwa Medicare na **131 272** kwa Child Support. Tujulishe ikiwa unahitaji mkalimani, na tutapanga mmoja kwa bure
- tembelea kituo cha huduma.

Kumbuka: simu kutoka simu yako ya nyumbani kwenda nambari za simu za '13' kutoka popote nchini Australia zinatozwa kwa kiwango kamili. Kiwango hicho kinaweza kutofautiana kutoka bei ya simu ya mtaa na kinaweza pia kutofautiana na watoa huduma wa simu. Simu kwa nambari za simu za '1800' kutoka simu yako ya nyumbani ni bila malipo. Simu kutoka simu za umma na za mkononi zinaweza kupimwa kwa muda wao na kutozwa kwa kiwango cha juu zaidi.

Kanusho

Taarifa iliyomo katika chapisho hili inakusudiwa kama mwongozo pekee wa malipo na huduma. Ni wajibu wako kuamua kama ungependa kuomba malipo na kufanya maombi kuhusiana na hali yako mahususi.



Parenting Payment

Parenting Payment is income support for parents or guardians to help with the cost of raising children.

Parenting Payment is a separate payment from Family Tax Benefit and Parental Leave Pay. There are also other payments for families you may be able to get.

Eligibility for Parenting Payment

Parenting Payment is paid to the principal carer of a child.

Only one parent or guardian can get the payment.

You may get Parenting Payment as a parent, grandparent, or foster carer, if any of these conditions apply:

- you are single and care for at least one child aged less than 14 years of age.
- you have a partner and care for at least one child aged less than 6 years of age.

To get this payment, you also need to meet these rules:

- the income and assets of both you and your partner (if you have one) are below certain amounts
- you meet the residence requirements
- you meet mutual obligation requirements if needed.

Payment rates for Parenting Payment

The amount of Parenting Payment you get depends on your family situation. The rates are updated on 20 March and 20 September each year. For the latest rates go to servicessaustralia.gov.au/parentingpayment

Income and assets tests for Parenting Payment

The amount of Parenting Payment you get depends on the income and assets of both you and your partner (if you have one).

An asset is any property or possession you own either in part or in full. It includes assets you hold, outside Australia and money and debts owed to you. The income and assets tests are updated on 20 March, 1 July and 20 September each year.

For the latest rates go to servicessaustralia.gov.au/parentingpayment

How to claim

You can't submit a claim for Parenting Payment before the birth of a child. We generally assess your Parenting Payment from the date you submit your claim and documents.

We can backdate your payments if you submit your claim and documents within either 4 weeks of:

- your child's birth
- the date the child came into your care.

You can apply for this payment online. For more information go to servicessaustralia.gov.au/parentingpayment

For more information

- go to servicesaustralia.gov.au/parentingpayment for more information in English
- go to servicesaustralia.gov.au/ftb for more information about Family Tax Benefit in English and other languages
- go to servicesaustralia.gov.au/yourlanguage where you can read, listen to or watch videos with information in your language
- call **131 202** to speak with us in your language about Centrelink payments and services
- call **132 011** for Medicare and **131 272** for Child Support. Let us know if you need an interpreter, and we will arrange one for free
- visit a service centre.

Note: calls from your home phone to '13' numbers from anywhere in Australia are charged at a fixed rate. That rate may vary from the price of a local call and may also vary between telephone service providers. Calls to '1800' numbers from your home phone are free. Calls from public and mobile phones may be timed and charged at a higher rate.

Disclaimer

The information contained in this publication is intended only as a guide to payments and services. It's your responsibility to decide if you wish to apply for a payment and to make an application with regard to your particular circumstances.